THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/2

KISWAHILI 2

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 3 **Jumatatu, 08 Mei 2017 asubuhi**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (9)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka sehemu A, B, C na D. Katika sehemu E, swali la **tisa (9)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.

AC17023
Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

SEHEMU A (Alama 20)

FASIHI KWA UJUMLA

1. Kwa kutumia mifano, elezea tofauti nne kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili.

2. Lengo la hadhira ni kuipa uhai kazi ya fasihi simulizi. Elezea dhima tatu za hadhira katika utanzu wa hadithi na dhima mbili za hadhira katika utanzu wa vitendawili.

SEHEMU B (Alama 20)

USHAIRI

Kimbunga	-	**Haji Gora**
Mapenzi Bora	-	**Shaaban Robert**
Chungu Tamu	-	**Theobald A. Mvungi**
Fungate ya Uhuru	-	**Mohamed S. Khatibu**

3. "Uongozi mbovu ni kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora." Jadili uhalisia wa kauli hii kwa kutoa mifano minne kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

4. "Ushairi ni msingi wa maneno yenye hekima kwa jamii ya leo". Thibitisha usemi huo kwa kutoa hoja nne kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

SEHEMU C (Alama 20)

RIWAYA

Usiku Utakapokwisha	-	**Mbunda Msokile**
Kufikirika	-	**Shaaban Robert**
Mfadhili	-	**Hussein Tuwa**
Vuta N' kuvute	-	**Shafi Adam Shafi**

5. "Mitazamo ya waandishi wa kazi za fasihi hutofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine." Kwa kutumia hoja nne kwa kila kitabu, bainisha mitazamo ya waandishi wawili kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.

6. "Dunia ni tambara bovu." Thibitisha usemi huu kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

SEHEMU D (Alama 20)

TAMTHILIYA

Kwenye Ukingo wa Thim	-	**Ebrahim Hussein**
Morani	-	**Emmanuel Mbogo**
Kivuli Kinaishi	-	**Said Mohamed**
Nguzo Mama	-	**Penina Muhando**

7. "Mapenzi ya kweli ni jawabu la migogoro mingi katika jamii." Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma.

8. Majibizano ni kipengele muhimu katika kuumba na kubeba wazo la mwandishi. Kwa kutumia hoja tatu kwa kila kitabu, onesha jinsi majibizano yalivyotumiwa na waandishi kujenga na kupendezesha kazi zao kupitia tamthiliya mbili ulizosoma.

SEHEMU E (Alama 20)

USANIFU WA MAANDISHI

9. Soma matini ifuatayo kisha bainisha vipengele vya fani vilivyotumika.

Kulikuwa kimya kwa muda. Wote wakanyamaza. Lakini ghafla mtu mwingine akashtuka na kusema, "Hawana shida bwana..." Uzuri wote wa UDA ulisahauliwa huko. Maskini UDA! Gari halikutokea. Baada ya muda kidogo ikasikika sauti kali "pyaaa!" Aligeuza shingo nyuma hakuna kitu. Kulia, hapana. Ni kushoto mwa kijumba kimoja karibu na kituo cha basi waliposimama. Kuna mtu mmoja alikuwa anagalagala, baiskeli kule! Miguu juu!

'Ondoa injinikiuno yako we! Bladi ful!" Alisikika mtu mwenye gari lililomgonga akifoka. Akalikodolea macho kwa nguvu na hasira gari hilo lililokuwa likilamba lami na kuyamaliza magurudumu yake. Limekwenda halina namba. Hakujua.....

Mhuni mmoja naye akamshambulia aliyegongwa, "Mwanaharamu we! Huangalii unapopita? Eee? Unafikiri mkokoteni huo? Ungefia mbali huko. Stupid!" Buricheka, akaguna akashangaa...machozi yakamtwaa machoni. "Kila mtu ana matatizo yake", aliwaza. Mji una namna mbalimbali ya kuwachachia watu. Simba akizidiwa hula majani. Hatimaye gari la UDA la kwanza lililotarajiwa kuwachukua watu kutoka Kona ya Bwiru kuwapeleka Mwanza mjini likaja. Mikikimikiki ikaanza! Watu walisukumana! Kila mtu aligombea nafasi mithili ya mbuzi wanaoswagwa kuingia zizini. Katika harakati hizo, mtu mmoja alichukuliwa fedha kutoka mfukoni.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

"Nimeporwaaaa-aa-aa, nimeporwaa, jamani". Watu hawakujali. Ohooo. "Unaleta gozigozi? Watakuiba hata wewe mwenyewe! bwege wewe." Kondakta wa basi hilo alifoka. Kama ilivyo ada sikio halilali njaa. Mtu mwingine akadakia. "Ah, shauri yako we mshamba wa kijijini." Buricheka aliwaza kidogo aliposikia hayo. "Dunia tambara bovu kweli" alijisemea.

Wakati huo huo, kuna mtu alikuwa anapanda basi kupitia dirishani, na alimkanyaga Buricheka begani. Buricheka akasonya lakini hakuna aliyemjali. Kwa hakika, asingethubutu kuparura mkono wake juu ya hili jitu la miraba minne kwani lingemcharanga na kumtafuna mbichimbichi. Hofu ikatawala moyoni mwake tena. Watu wengine walitaka kushuka. "Oya we mama toa makalio yako njiani tunashuka". Kijana mmoja alionekana amenyoa nywele kama ugiligili wa jogoo alibwatuka.! Mama naye kumbe mtata! Akamjibu, "Shuka zenyewe ziko wapi? Peleka fito zako huko. Watu walicheka kwenye basi wakampongeza mama kwa kumyoosha huyo kijana mkosa adabu.

Vituko vya UDA viliendelea. Baada ya dakika chache akaja mama mmoja mgonjwa. Yeye aliomba msaada kuwa apite mlango wa mbele karibu na kule anapokaa dereva. Akasukumwa kwa nguvu na kondakta, akaanguka huku akifokewa kuwa hii siyo gari ya wagonjwa. "Soma juu ya mlango". Kwa kweli, "Asiyekujua hakuthamini!" Zimwi likulalo hadi mwisho halikujui!

Kwa mbele kulikuwa kijana mwingine aliyetaka kushuka. "Pisha...pisha...pisha!" Waliokuwa karibu nae walimwita Jaluo. Lakini Jaluo akalalamika kwa nguvu, "Musee ona kwisa kanyaga mimi? Dunia musima inasangilia amani wewe inakanyagana?" "We Jaluo toa kelele zako hapo unafikiri basi hili la baba'ko?" Kijana mwingine alidakia. Jaluo alikunja uso ukawa na makunyanzi kama goti la mbuzi na kufoka, "Siku mingine tafyeka koromeo lako". Watu walicheka kwenye basi na hapo Buricheka nae akaangua kicheko.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org